TAARIFA YA UANZISHAJI MASOKO YA MADINI ILIYOSOMWA NA PROF. SIMON MSANJILA KWENYE UZINDUZI WA SOKO LA DHAHABU LA MKOA WA GEITA TAREHE 17 MACHI 2019.

Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mheshimiwa Dotto M. Biteko (Mb.), Waziri wa Madini,

Mh. Dkt Medadi Kalemani, Waziri wa Nishati,

Waheshimiwa Manaibu Mawaziri Mliopo,

Mh. Robert Gabriel, Mkuu wa Mkoa wa Geita,

Waheshimiwa wakuu wa mikoa mliopo,

Ndugu Denis Bandisa, Katibu Tawala Mkoa wa Geita,

Waheshimiwa wakuu wa Wilaya,

Prof. Idris Kikula, Mwenyekiti wa Tume ya Madini,

Prof. Shukrani Manya, Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini,

Katibu Tawala wa Wilaya,

Wakurugenzi wa Wilaya,

Watendaji wa Wizara na Tume ya Madini

Wawakilishi wa wachimbaji Madini

Wanahabari

Wageni waalikwa

Mabibi na Mabwana.

HABARI ZA MCHANA

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kukutana hapa leo, katika uzinduzi wa soko la Madini ya dhahabu mjini Geita. Naomba pia nikushukuru wewe mwenyewe kwa kukubali kuja huku Geita kutufungulia soko hili la kwanza la aina yake, soko la dhahabu. Naomba pia uniruhusu niwashukuru sana wananchi wote wa mkoa wa Geita chini ya uongozi wa Mkuu wa Mkoa wa Geita kwa mwitikio wao wa haraka na chanya katika kujenga soko hili na hata leo tunawaona hapa wakiwa wamefika kwa wingi kushuhudia soko lao likizinduliwa. Naomba pia niwashukuru wengine wote waliokubali mwaliko wetu na kusafiri kokote walikotokea na kufika hapa kuungana nasi katika tukio hili muhimu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Tarehe 22/01/2019, Mh. **Dkt.John Pombe Joseph Magufuli,** Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania,alifungua na kushiriki mkutano Mkuu wa Kisekta wa wachimbaji wadogo uliolenga kusikiliza kero na changamoto zinazoikabili sekta hii ya madini hasa kwa wachimbaji wadogo. Kupitia mkutano huo, Mh. Rais alipokea kero mbalimbali za wachimbaji wadogo, na kutoa maelekezo ya namna ya kuziondoa kero hizo. Moja ya kero iliyoainishwa na Wachimbaji wadogo, ni ukosefu wa masoko ya uhakika na rasmi ya Madini katika maeneo mbalimbali wanayofanyia shughuli zao za uchimbaji. Wadau hawa walieleza kuwa, ukosefu wa masoko rasmi na ya uhakika ndio sababu kubwa inayowafanya watoroshe madini na kuuza katika masoko yasiyo rasmi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Baada ya kikao hicho cha sekta, wewe mwenyewe ulitufungulia kikao tarehe 26/01/2019 cha viongozi mbalimbali wa serikali kilicho wajumuisha Mawaziri wa Wizara mbalimbali, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala Mikoa na wawakilishi toka Wizara na Tume ya Madini, lengo likiwa ni kujadili mikakati na pia kutoa maelekezo ya namna ya kuondoa kero ya ukosekanaji masoko ya madini nchini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Napenda kukutaarifu kuwa, mikoa karibia yote tayari imeshaanza taratibu za uanzishaji masoko ya madini ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo na majengo yatakayotumika kwa masoko ya madini, na baadhi ya mikoa hiyo ipo hatua za mwisho kukamilisha vigezo mbalimbali vikiwemo vya kiusalama na miundombinu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wizara inaupongeza Mkoa wa Geita kwa hatua hii muhimu waliyoifikia kwa sababu, Mkoa huu umebarikiwa kuwa na shughuli nyingi sana za uchimbaji wa madini, hasa ya dhahabu. Vilevile Mkoa huu, una wachimbaji wengi sana wadogo na wa kati, lakini pia na uchimbaji mkubwa. Pamoja na uchimbaji huo, mkoa huu unaongoza kwa shughuli za uchenjuaji wa dhahabu (*processing*) unaotumia teknolojia mbalimbali zikiwemo za *Mercury amalgamation*, *Vat Leaching, Elution, Carbon-In-Leach* (CIL) na *Carbon-In-Pulp* (CIP).

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Hadi kufikia mwezi Februari 2019, Mkoa huu wa Geita una Leseni kubwa za Uchimbaji wa Madini (*SML*) **2**, Leseni za Uchimbaji wa Kati (*ML*) **48**, Leseni za Uchimbaji Mdogo wa Madini (*PLM)***1119,** Leseni za uchenjuaji wa Madini ya dhahabu **47,** Leseni kubwa za biashara ya Madini ya dhahabu (*Dealers Licence)* **18**, Leseni ndogo za biashara ya madini (*Gold Brokers)* **113**. Hii inaonesha kwa kiasi gani soko hili lilikuwa linahitajika sana hapa. Aidha kutoka katika mkoa huu huu wa Geita, Wizara kupitia Tume ya Madini, inaendelea kupitia maombi **258** ya leseni za uchenjuaji (*VAT leaching & Elutionplants), maombi **12*** ya leseni kubwa za biashara ya madini (*Gold Dealers Licence applications) na maombi **86** ya* leseni ndogo za biashara ya madini (*Gold Brokers Licence applications*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Kwa upande wa makusanyo ya serikali, maduhuli yatokanayo na uzalishaji wa Madini katika mkoa huu umeongezeka kutoka **TZS 24.54 bilioni** kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na kufikia **TZS 114.78 bilioni** kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Ongezeko hili ni mwitikio chanya wa mabadiliko mbalimbali ya kisera ya kisheria ambayo yamekuwa yakitekelezwa na serikali ya Awamu ya Tano. Mathalani katika kipindi cha Januari hadi Juni 2018 uzalishaji wa madini ya dhahabu ulipanda kutoka **Kg 662** yenye thamani **Tsh 48.58 bilioni** wakati kipindi cha Julai hadi Disemba 2018 hadi **uzito** wa **Kg 973** wenye thamani ya **Tsh 76.89 biolioni**. Hii pia ilipelekea kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli kutoka **Tsh 3.32 bilioni**

hadi kufikia **Tsh 5.36 bilioni** kwa wachimbaji wadogo, wakati na wachenjuaji katika kipindi hicho

Katika mwaka huu wa fedha 2018/19 Ofisi ya Madini Geita imepangiwa kukusanya kiasi cha shilingi **85 bilioni**. Hadi kufikia machi 15, 2019 jumla ya **Tsh 91.75 bilioni** za maduhuli zimekusanywa ambayo ni sawa na **asilimia 107.95** ya lengo la mwaka. Hivyo soko hili sasa litapandisha zaidi makusanyo ya serikali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Katika Soko hili Kuu la Madini Geita, kutakuwa na sehemu ya ukaguzi na uthaminishaji Madini, kutakuwa na eneo la soko (auction and exchange), na kutakuwa na eneo ambalo miamala itafanyika na vibali mbalimbali vitatolewa. Eneo hili la tatu tutaliita ***Clearing House*** ambalo litakuwa maalumu kwa kukamilisha miamala na hivyo kutakuwa na huduma za Benki, Bima, TRA, Tume ya Madini, huduma za forodha na uhifadhi wa madini (*Minerals storage*).

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Uwekezaji miundombinu katika jingo la soko hili la dhahabuhadi kufikia hali ya sasa linapozinduliwa umeghalimu uwekezaji wa takribani Tsh Milioni 542. Wizara inawapongeza inawapongeza sana Mkoa wa Geita kwa uwekezaji huu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Ni matumaini yangu baada ya kushuhudia leo Geita wamefanikiwa Mikoa yote, hasa yenye uzalishaji mkubwa wa madini, itakamilisha uanzishaji masoko ndani ya muda mfupi ujao.

Naupongeza tena uongozi wa Mkoa wa Geita ukiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa **Mhandisi Robert Gabriel** na Katibu Tawala **Ndugu. Denis Bandisa,** viongozi na wadau wote wa madini kwa kutekeleza maagizo ya serikali kwa vitendo na haraka.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naomba kuwasilisha;

MWISHO.